# HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 60 YA MUUNGANO WA TANZANIA,

**TAREHE 25 APRILI, 2024, DODOMA**

***Ndugu Wananchi,***

Panapo majaaliwa, kesho tarehe 26 Aprili, 2024, Muungano wetu utatimiza miaka 60 tangu uasisiwe, jambo lenye muhimu sana katika historia yetu. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kheri zote na baraka alizotujaalia, na kutuwezesha kuifikia siku hii.

Nitumie fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuzindua Maadhimisho haya, tarehe 14 mwezi huu, na kwa ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwenye shughuli zote za Maadhimisho. Nimshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwenye dhamana ya masuala ya Muungano. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa uratibu mzuri wa maadhimisho tunayoyahitimisha kesho.

Mimi binafsi, namshukuru Mungu kwa kuinasibisha historia ya maisha yangu na Muungano wetu. Pamoja na kuyaishi masuala ya Muungano kama raia wengine, nimebahatika pia kufanya kazi katika kuuimarisha Muungano; **kwanza,** kama Mjumbe wa Kamati ya Pamoja ya kutatua Changamoto za Muungano, **pili,** nikiwa Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Makamu wa Rais wa Tanzania anayeshughulikia masuala ya Muungano.**;** **tatu**, kama Makamu wa Rais, na sasa, nikiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hivyo basi, tunapokusanyika sehemu mbalimbali za nchi yetu kusheherekea na kuiadhimisha miaka 60, nimeona ni muhimu kuzungumza na Taifa kuhusu tunu hii ya Muungano na umuhimu wake.

***Ndugu Wananchi,***

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliundwa tarehe 26 mwezi wa nne mwaka 1964 ikiwa ni Muungano wa hiari wa nchi mbili huru: Jamhuri ya Tanganyika chini ya uongozi wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ikiongozwa na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume. Muda mchache ujao tunaadhimisha kutimia miaka 60 tangu kuanzishwa kwake. Katika hili, hatuna budi kukumbuka, kutambua, kupongeza na kuuenzi mchango mkubwa wa waasisi wetu ambao daima waliamini katika

umoja. Hatuna budi pia kuwapongeza viongozi wa Awamu zote za Serikali zetu mbili waliofuatia, kwa uongozi wao katika kuuenzi, kuudumisha na kuuimarisha Muungano wetu. Tunawashukuru sana Viongozi wetu hao.

***Ndugu wananchi,***

Kila ninapopata fursa ya kuzungumzia Muungano wetu, fikra zangu hutawaliwa na picha ya vijana wanne kutoka pande zote mbili za Muungano. Vijana hao, wawili wa kiume na wawili wa kike, waliomsaidia Mwalimu Julius Nyerere kuchanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar kutoka kwenye vibuyu viwili tofauti, kwa kuumimina kwenye chungu kimoja, kitendo kilichoashiria kuundwa kwa Taifa jipya, yaani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jinsi udongo ulivyo, ni vigumu sana kuuchambua na kuweza kuutenganisha uliotoka Zanzibar na ule uliochotwa Tanzania Bara. Baada ya kuuchanganya, hakuna teknolojia inayoweza kuurudisha udongo ule kwenye hali yake ya awali katika vibuyu viwili tofauti. Kwa maana nyingine, kitendo cha kuchanganywa kwa udongo kiliashiria dhamira ya kujenga muungano wa kudumu.

Muungano wetu ni maalumu na wa kipekee, uliojengwa katika misingi ya utu, udugu, na umajumui wa Afrika (*Pan-Africanism*), umeweza kushinda majaribu mengi ya kuuvunja,

na vilvile umefanikiwa kudumu hadi sasa. Nchi nyingi ziliwahi kufanya majaribio ya kuungana, bila ya mafanikio. Katika kuelezea upekee wa Muungano huu, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema maneno yafuatayo, naomba kunukuu: ***"Tanzania ni lulu ya pekee kabisa katika historia ya Afrika huru. Nchi nyingine zote ni za kurithi kutoka katika Ukoloni. (Lakini) Tanzania ni ya kuundwa na sisi wenyewe, kwa hiari yetu wenyewe, baada ya kukomboa sehemu (zote mbili za Muungano) kutoka katika Ukoloni."*** Kwa upande wake, Sheikh Abeid Amani Karume akiuzungumzia Muungano huu, aliwahi kusema, nanukuu ***''Muungano wa Tanganyika na Zanzibar una thamani kubwa kwetu sisi Waafrika''.***

Viongozi hawa pamoja na wasaidizi wao, waliongozwa na busara, hekima na ushujaa katika kutuleta pamoja. Vilevile, viongozi wa awamu zote zilizofuata wamelipa suala la Muungano uzito mkubwa.

***Ndugu wananchi,***

Inawezekana baadhi ya Watanzania wakajiuliza, iliwezekanaje Muungano huu ukawepo, na umewezaje kudumu miaka yote hii? Majibu ya maswali hayo ni muhimu kwa kutambua kwamba zaidi ya robo tatu ya Watanzania wa leo, wamezaliwa baada ya Muungano. Maelezo kuhusu maswali hayo yapo mengi, lakini kwa muktadha wa leo

nitazungumzia mambo makubwa **matatu** yaliyoufanya Muungano wetu udumu na kuimarika.

Jambo la **kwanza**, ni imani na dhamira ya dhati waliyokuwa nayo waasisi wa Muungano, Hayati Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume. Viongozi hao walikuwa mstari wa mbele katika kudai uhuru kupitia Vuguvugu la Umajumui la Afrika Mashariki na Kati, yaani *Pan African Movement of Eastern and Central Africa*, au kwa ufupi PAFMECA. Lengo la PAFMECA lilikuwa kujenga umoja, mshikamano na ushirikiano miongoni mwa watu wa Afrika waliokuwa chini ya utawala wa kikoloni wakidhamiria kuunganisha nchi zao mara baada ya kupata uhuru. Mnamo mwaka 1959, Sheikh Karume, alikuwa mwenyeji wa mkutano wa PAFMECA uliofanyika Zanzibar kwa mafanikio makubwa.

Mwalimu Nyerere kwenye moja ya mikutano ya PAFMECA aliwahi kusema hivi, naomba kunukuu: ***"Lazima tuzisumbue ofisi za wakoloni kwa nia si ya kudai uhuru wa Tanganyika, kisha Kenya na Uganda halafu Zanzibar, lakini kwa nia ya kutaka uhuru wa Afrika Mashariki kama Muungano mmoja wa kisiasa".*** Mwisho wa nukuu. Kwa hivyo basi, uamuzi wa kuziunganisha nchi zetu halikuwa jambo la ghafla, bali lililotokana na dhamira ya dhati ya kutaka nchi zetu ziungane tangu wakati tunadai uhuru.

**Jambo la pili** ni udugu wa kihistoria. Watu wa Zanzibar na watu wa Tanganyika walitenganishwa na mipaka ya ukoloni tu, lakini kwa asili walikuwa ni watu wa jamii moja. Wengi wao, wanapofuatilia nasaba zao, wanajikuta kuwa chimbuko lao ni kutoka upande mmoja au mwingine wa Muungano. Kwa mfano, ndugu zangu wengi wa Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara, Morogoro, Mwanza, Shinyanga na Tabora wana ndugu zao wa asili kule Zanzibar. Hali hii pia imechangia sana kuudumisha Muungano wetu.

**Jambo la tatu**, ni umadhubuti wa viongozi waasisi waliotanguliza mbele maslahi ya watu na Taifa. Kujitolea kwao kwa manufaa ya wengi, vimechangia sana kuwepo kwa Muungano huu. Uamuzi wa kuziunganisha nchi zao muda mfupi baada ya uhuru, bila kujali kupoteza nyadhifa au mamlaka yao, unadhihirisha dhamira na imani yao katika kuunganisha watu, na kuliunganisha Bara la Afrika.

***Ndugu wananchi,***

Kudumu kwa Muungano huu kumetokana na dhamira ya waasisi wa Muungano na viongozi waliofuata, kusimamia misingi na malengo ya kuasisiwa kwake. Sababu nyingine ni udugu wa kihistoria, uwepo wa lugha ya Kiswahili na wananchi kuukubali Muungano huu kuwa ni wao. Kwa hiyo, ni Muungano wa kisiasa uliojengwa kwenye misingi ya historia ya kijamii.

***Ndugu zangu***, katika kipindi cha uhai wa Muungano, wananchi wamehama au kuhamia kutoka upande mmoja wa Muungano kwenda upande mwingine. Wamejenga, wameoa na kuolewa na kuleta kizazi cha watanzania, wanaendesha shughuli zao za maisha bila ya kubughudhiwa.

Muingiliano wa shughuli za kijami na kiuchumi umeongeza kasi kwa wananchi kutembeleana kwa wingi. Kuna wanaosafiri kwa majahazi kutoka Unguja na Pemba kwenda Pangani, Mkwaja, Saadani, Bagamoyo, Mafia, Kilwa na kadhalika; na wapo wanaotoka Pwani ya Bara na kuingia Zanzibar kupitia bandari za Fuoni, Kizimkazi, Fumba, na Mkokotoni. Vilevile, kuna wanaotumia boti za kisasa au ndege pia. Wote hao, bila Muungano, wangelazimika kusafiri kwa utaratibu mgumu zaidi ambao huenda ungehusisha kutafuta visa, kutumia hati za kusafiria na hata kupata vibali vya ajira upande wowote ule wa Muungano.

Sababu nyingine ya Muungano wetu kudumu ni uwepo wa Tume ya Pamoja chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, inayosikiliza na kutatua changamoto za Muungano kila zinapojitokeza. Katika ya mwaka 2021 hadi sasa, hoja 15 kati ya 18 zimeshapatiwa ufumbuzi. Tume hiyo inafanya kazi kubwa ya kulinda dhamira ya dhati ya kuudumisha Muungano wetu.

Ni wajibu wetu kuendelea kuweka mazingira mazuri zaidi ya watu kushirikiana, kujenga umoja na mshikamano wa Kitaifa, ili Muungano wetu udumu vizazi hadi vizazi na kuleta manufaa zaidi kwa watu wetu.

Pamoja na kuwaunganisha wananchi na kuimarisha mahusiano mazuri, Muungano umetuwezesha kulinda Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, lakini pia kwa umoja wetu, na kupitia jeshi letu, tumeweza kulinda mipaka ya taifa letu. Ninafuraha leo kuwahakikishia kwamba, mipaka yetu, uhuru wetu, na mapinduzi yetu, vyote viko salama ndani ya Muungano wetu.

Nafarijika kwamba Jeshi letu la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, JWTZ ifikapo mwezi Septemba mwaka huu nalo linatimiza miaka 60 tangu kuundwa kwake

Wajibu wetu ni kuendelea kuviimarisha vyombo vya ulinzi na usalama ili viendelee kutimiza jukumu la kulinda mipaka na usalama wa raia na mali zao kwa ufanisi mkubwa. Hapa nataka kukumbusha kwamba, mlinzi wa kwanza wa usalama wa nchi ni mwananchi mwenyewe. Kila mmoja wetu awe macho na ashirikiane na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kubaini, kuzuia na kukabiliana na matishio kwa usalama wa jamii zetu na nchi kwa ujumla.

Muungano wetu pia umetuwezesha kuimarisha utawala bora katika pande zote za Muungano. Kwa nyakati tofauti, Muungano umetoa nafasi kwa mageuzi makubwa kufanyika ndani ya nchi. Baadhi ya mageuzi hayo ni pamoja na kutambuliwa kwa haki za binadamu kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar; kurejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992; na kuanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Vilevile, Mihimili mitatu ya Dola imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa katiba, kwa kushirikiana na bila muingiliano.

Muungano wetu pia uliwezesha vyama vya ASP na TANU kuungana na kuanzishwa Chama cha Mapinduzi mwaka 1977. Jambo hili, liliweka msingi wa nchi yetu kuwa na vyama vya siasa vya kitaifa, na vyama vinavyoakisi sura ya Muungano wetu.

***Ndugu zangu,*** Ili tuweze kujenga Muungano ulio imara zaidi, Serikali immekuja na falsafa ya **maridhiano, kustahimiliana, tuweze kubadilika, na kwa pamoja tujenge upya Taifa letu (maarufu kama R4)**. Kupitia falsafa hio, tumefanya mapitio ya mfumo wa haki jinai; kuhakikisha uhuru wa kujieleza,na vyama vya siasa kufanya shughuli zao

kwa uhuru. Aidha, kupitia mazungumzo na ushirikishwaji, tumefanya mabadiliko kwenye sheria zetu za uchaguzi, sheria ya vyama vya siasa na sheria ya Tume ya Uchaguzi.

Katika diplomasia, Muungano umeiwezesha Tanzania kuwa na ushawishi mkubwa zaidi kikanda na kimataifa. Tumeweza kunufaika na kukuza uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi nyingine, na Nchi yetu na Taasisi za Kimataifa kwa manufaa ya pande zote za Muungano.

Nchi yetu ilishiriki kikamilifu katika harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika, na usuluhishi wa migogoro katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Pia, kupitia mwelekeo wetu wa sasa wa Diplomasia ya Uchumi, tumeweza kuvutia mitaji, uwekezaji, teknolojia na kupata soko la bidhaa na huduma zetu.

***Ndugu wananchi;***

Wakati tunaungana, kiuchumi, nchi zetu, Tanganyika na Zanzibar, zilikuwa katika kiwango duni cha maendeleo na wananchi wengi walikuwa katika hali ya umasikini. Sekta za uzalishaji hususan kilimo kilikuwa chenye tija ndogo na hapakuwa na miundombinu ya kutosha ya usafiri na usafirishaji. Huduma za kijamii, elimu, afya, maji na umeme pia zilikuwa ni adimu na za kibaguzi.

Kwa hiyo, jukumu la kwanza baada ya Muungano, lilikuwa ni kujenga uchumi endelevu na wenye kuwanufaisha wananchi wote bila ubaguzi kwa kuimarisha na kupanua huduma za kiuchumi na kijamii na hivyo kuongeza kipato cha wananchi. Jitihada zilizofanywa ndani ya miaka hii 60 zimesaidia kukuza Pato la Taifa, kufikia **Shilingi Trilioni 170.3 kwa takwimu za** mwaka 2022, na pato la mtu mmoja mmoja kufikia wastani wa **shilingi milioni 2.8** kwa mwaka 2022. Nafarijika kwamba, kwa sasa nchi yetu imefikia uchumi wa kati, katika ngazi ya chini, na jitihada zetu zote sasa ni kufikia uchumi wa kati, ngazi ya juu. Vilevile, wastani wa umri wa kuishi *(life expectancy)* wa Mtanzania umeongezeka kutoka wastani wa miaka 45 mwaka 1964 hadi wastani wa miaka 67 mwaka 2024.

Aidha, uhamiaji wa wananchi kutoka upande mmoja wa Muungano kwenda kuishi upande mwingine, sio tu umeleta msisimko wa kiuchumi, bali pia umekuwa na athari chanya kwenye tamaduni zetu.

***Ndugu Wananchi,***

**Sensa** ni moja kati ya mambo ya Muungano. Hadi sasa, zimefanyika sensa za watu na makazi mara 6, Sensa ya kwanza ilionesha Tanzania kuwa na watu Milioni 9.6 na ile ya mwisho ya 2022 imetuonesha idadi ya Watanzania kuwa milioni 61.741. Taarifa hizi za Sensa zina msaada mkubwa

kwa mipango ya kiserikali., na kutuongoza katika matumizi ya rasilimali, na kuimarisha uwakilishi wa wananchi.

***Ndugu wananchi;***

Serikali zetu mbili zimeendelea kuibua na kutekeleza programu na miradi mbalimbali inayolenga kupunguza umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii kwa pande zote mbili za Muungano. Programu mojawapo inayotekelezwa na pande mbili za Muungano ni Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF, uliotekelezwa kwa Awamu 3. Tathmini inaonesha kwamba uwezo wa kaya kumudu gharama za mahitaji ya msingi umeongezeka, vilevile matumizi ya pembejeo yameongezeka na hivyo kuongeza tija kwenye kilimo, na matumizi ya huduma za afya pia yameongezeka, na mahudhurio shuleni kwa watoto nao umeongezeka.

Miradi mingine iliyotekelezwa pande zote mbili ni pamoja na Programu ya Usimamizi wa Bahari na Pwani (*MACEMP)*; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Sekta ya Mifugo (*ASDP – L).* Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani ya Mazao na uboreshaji wa huduma za Fedha Vijijini (*MIVARF);* Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga *(ERPP)*; na, Mradi wa

Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya Pwani (LDCF).

Programu nyingine inayoendelea kutekelezwa pande mbili za Muungano ni Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF), mfumo wa Wabunge, ambao umewanufaisha wananchi katika sekta za afya, maji, ajira, elimu na miundombinu.

***Ndugu Wananchi***, mazingira mazuri yaliyojengwa na Muungano wetu yamewezesha wanafunzi katika ngazi ya elimu ya juu kupata elimu bila ubaguzi. Itakumbukwa kuwa baada ya uhuru, chuo kikuu pekee kilikuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na Zanzibar haikuwa na Chuo Kikuu. Kupitia Muungano, vijana wa Kizanzibari walipata fursa ya elimu ya juu katika Chuo hicho na vyuo vingine Tanzania Bara.

Ninafarijika kwamba, miaka **60** baada ya Muungano tunavyo vyuo vikuu **49** vikiwemo **19** vya umma na **30** vya binafsi. Kati ya vyuo hivyo, **46** viko Tanzania Bara na **3** viko Tanzania Zanzibar. Vyuo hivi vinatoa fursa za masomo kwa wanafunzi kutoka pande zote za Muungano, ambapo kwa Mwaka 2023/24, kulikuwa na jumla ya wanafunzi wa elimu ya juu **240,523**, ikilinganishwa na wanafunzi **14** tu waliokuwepo wakati nchi zetu zinaungana. Zaidi ya hapo, Serikali ya Tanzania imeendelea kutoa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wa pande zote za Muungano. Tangu kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo mwaka 2004 wanafunzi

wapatao **705,622** wamepatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi **Trilioni 6.69,** ambapo wanufaika wanawezeshwa kusoma kwenye vyuo vya Serikali na vyuo binafsi pia.

***Ndugu wananchi,***

Suala la usawa wa kijinsia limepewa umuhimu katika Muungano tangu siku ya kwanza ya Muungano wenyewe. Kama nilivyoeleza hapo awali kuhusu vijana wa kike na wa kiume walioshiriki kwenye kuchanganya udongo. Hii ilikuwa ni ishara kwamba, Muungano wetu ulidhamiria kujenga Taifa lenye usawa. Suala la usawa wa kijinsia zote liliingizwa kwenye Katiba, hatua iliyowezesha uwakilishi wa wanawake Bungeni kuongezeka kutoka watatu tu mwaka 1964 wakati wa Bunge la kwanza la Muungano, hadi sasa kufikia wabunge wanawake **148** sawa na **37.75%** ya wabunge wote **392** tulionao sasa. Aidha, wakati huo, hapakuwa na mwanamke yeyote kwenye uongozi wa mihimili ya dola, yaani Serikali, Bunge na Mahakama. Leo hii, kati ya mihimili mitatu ya dola, wanawake wanaongoza mihimili miwili, Serikali na Bunge, jambo linalothibitisha kuendelea kuimarika kwa usawa wa kijinsia.

***Ndugu Wananchi,***

Umoja na mshikamano wetu umetufanya tuweze kukabiliana na changamoto zote zinazotukumba kama Taifa la Tanzania. Mwishoni mwa miaka ya sabiini na kwenye

miaka ya themanini tulikumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukame na njaa. Kama haikutosha, mtikisiko na anguko la uchumi duniani ulisababisha kupanda kwa bei ya mafuta na vyakula ulimwengu mzima, hali iliyovuruga uchumi wetu kwa kiasi kikubwa. Aidha, mwaka 1977 Jumuiya ya Afrika Mashariki ilivunjika, na hivyo kuilazimu Serikali kugharamia upatikanaji wa huduma zilizokuwa zinatolewa na Jumuiya hiyo. Katikati ya changamoto hizo, kukazuka vita dhidi ya Nduli Idd Amin, vilivyosababisha fedha zilizotengwa kwa maendeleo yetu, na rasilimali nyengine kuelekezwa kwenye kugharamia vita hivyo.

Vilevile, kwa nyakati mbalimbali, katika soko la Dunia tulikumbana na anguko kubwa la bei za mazao yetu ya biashara kama vile chai, mkonge, kahawa, karafuu na pamba, hali iliyoathiri ukuaji wa uchumi wetu uliokuwa unaimarika vizuri. Aidha, magonjwa kama vile UKIMWI, Kipindupindu, Homa ya mafua ya ndege, na hivi karibuni UVIKO 19, nayo yalitikisa Taifa letu.

Kwa upande mwingine, miaka ya 2001 hadi 2007 tulipata changamoto ya kisiasa Zanzibar, iliyosababisha baadhi ya washirika wetu wa maendeleo kusitisha misaada.

Mambo haya yote, yalitufanya tuunge nguvu kitaifa, tuimarishe umoja na mshikamano wetu, uliotujengea uwezo

wa kuhimili kadhia zote hizo, na kulivusha Taifa letu likiwa salama na imara zaidi.

***Ndugu zangu,*** kama tunavyojua, umoja wowote hauachi kuwa na changamoto. Kumekuwa na changamoto za kiuchumi, kisiasa na kijamii ambazo zilihitaji kutafutiwa ufumbuzi. Serikali zetu mbili zimeweka Mwongozo rasmi wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya Kushughulikia Masuala ya Muungano, ambapo mambo mengi yametafutiwa ufumbuzi. Tangu kuanzishwa kwa utaratibu wa vikao vya pamoja mwaka 2006, kumekuwa na mwenendo mzuri wa utatuzi wa changamoto zinazoibuka, na majadiliano ya Kamati hiyo yameimarisha zaidi Muungano wetu.

Kama tunavyofahamu, pamoja na kusimamia masuala ya Muungano, Ofisi ya Makamu wa Rais pia inaratibu na kusimamia utunzaji wa mazingira ndani ya nchini yetu. Ni jambo la kujivunia kwamba, tunapoadhimisha miaka 60 ya Muungano, nchi yetu imeendelea kuwa mstari wa mbele katika utunzaji wa mazingira, ambapo takribani asilimia 33 ya ardhi yote ya Tanzania imehifadhiwa.

Hivyo, nitumie fursa hii kuipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuhamasisha jamii ya Watanzania kutunza mazingira. Ninafahamu kwamba kama sehemu ya

maadhimisho haya hadi kufikia leo takribani miti 49,981 imepandwa. Nawapongeza sana wote walishiriki kwenye zoezi hili na nitoe rai kwa Watanzania kuwa utamaduni wa kutunza mazingira na kupanda miti uwe endelevu na uanzie katika ngazi ya familia.

***Ndugu zangu***

Katika kipindi cha miaka 60 nchi yetu imeendelea kuimarisha Mawasiliano kupitia vyombo vya habari, simu za mkononi na mitandao ya kijamii. Wakati tunaungana njia kuu za Mawasiliano za haraka tulizokuwa tukitegemea ni simu za mezani na zilikuwa katika familia chache sana. Leo hii kupitia Muungano wetu tumeweza kuimarisha mawasiliano, na hadi sasa takriban kila familia ina mtu mwenye simu ya mkononi na watoa huduma za simu wameongezeka.

Kwa sasa inakadiriwa jumla ya laini za simu zinazotumika ni zaidi ya milioni 72 na watoa huduma wameongezeka hadi watano ambao wameshaanza kutoa huduma zenye kasi ya 5G. Zaidi ya kutumia laini hizo kwa mawasiliano, vile vile kiasi cha laini milioni 53 zimesajiliwa kutumia huduma za kifedha kupitia simu za mkononi na hivyo kuwarahisishia Watanzania kufanya shughuli zao za kiuchumii na kijamii.

Maendeleo haya yamechangiwa na uamuzi wa Serikali kuanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote maarufu kama UCSAF wenye jukumu la kuimarisha miundombinu ya mawasiliano vijijini. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2009 UCSAF imeweza kujenga minara 1,435 iliyowezesha zaidi ya wananchi milioni 16 katika kata 1,306 na vijiji 3,838 kupata mawasiliano ya uhakika. Jitihada za Serikali kupitia UCSAF na sekta binafsi zimewezesha kuimarika kwa huduma za mawasiliano ambapo kwa sasa asilimia 98 ya Watanzania wanafaidika nchini kote.

**Haya ni Baadhi ya Matunda ya Muungano wetu.**

***Ndugu Wananchi;***

Ninapohitimisha hotuba yangu, niseme tu kwamba, Muungano wetu umetuimarisha zaidi kama Taifa, na kwamba Muungano wa Taifa letu unahitajika leo, kama ambavyo tuliuhitaji mwaka 1964. Hivyo basi, hatuna budi kuulinda Muungano huu kwa manufaa ya Watanzania wa kizazi cha sasa na Watanzania wa vizazi vijavyo.

Matokeo ya Sensa ya mwaka 2022 yanatuonesha kwamba idadi kubwa ya Watanzania ni vijana. Kwa kuzingatia hilo, uimara na uendelevu wa Muungano huu, uko mikononi mwenu vijana wetu. Ninawasihi sana vijana wote wa Tanzania muwe walinzi wa Muungano wetu. Kumbukeni

kuwa Muungano huu ni urithi na tunu ya Taifa letu, na ni tunu ya Afrika kwa ujumla.

Vile vile, niwasihi wanasiasa wenzangu kukumbuka kwamba Muungano ni wa watu. Nitoe rai kuwa siasa zetu zijikite kwenye kudumisha mafanikio yaliyopatikana katika miaka 60 ya Muungano, na tudhamirie kufanya siasa zenye kuleta maendeleo, kuwaunganisha watu, kuthaminiana, na kudumisha misingi ya utawala wa sheria.

Kwa wananchi wenzangu, kama nilivyosema mara kadhaa, ninarudia kusema kwamba, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja tu ulimwenguni, na ndio inayozaa Watanzania. Jamhuri hiyo ni yetu na Tanzania ndio kwetu hatuna kwengine ***katu, abadan.*** Ninawasihi kudumisha uzalendo kwa kuzidisha umoja na mshikamano wa Kitaifa. Tukifanya hivyo, tutaweza kuurithisha Muungano huu kwa vizazi vyetu, ukiwa imara zaidi.

**Mungu Ubariki Muungano Wetu!**

**Mungu Ibariki Tanzania;**

**Na Mungu aibariki Afrika!**